

USUKUKU KATIKA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA JAMII YA WAKINGA

Arnold Gawasike

Ikisiri

Usukuku ni dhana inayotumika sana katika taaluma ya isimu matumizi, hasa katika kipengele cha ukipatiaji na ujifunzaji wa lugha ya pili na au ya kigeni, ikiwa na maana ya ukomo wa mtu kuendelea kujipatia lugha baada ya balehe (Long, 1997). Makala haya kwa hiyo yanafasili na kuainisha dhana hii katika muktadha wa Kiswahili. Pili, yanapendekeza baadhi ya mbinu ambazo zinaweza kutumiwa na walimu wanaofundisha lugha ya pili ili kuwasaidia wajifunzaji kuondokana na tatizo la usukuku. Swali linaloibuliwa na kujibiwa na makala haya ni je, kuna ukomo wa ukipatiaji lugha kama wanavyodai Long (1997), Lardiere (1998) na Jiang (2000)?

1.0 Utangulizi

Wakati utafiti mpana kuhusu ukipatiaji lugha ya pili (kuanzia sasa L2) ukiwa umejikita zaidi katika mchakato wa ukipatiaji lugha pekee, tapo jingine limestahabali (*Specialise*) katika kuchunguza baadhi ya vipengele vya kiisimu ambavyo husukukishwa. Kwa mfano, Han (2009) katika Nadharia Teuzi ya Usukuku¹ anaeleza vipengele vya ukipatiaji lugha na usukukisho kwa kubainisha michakato yote miwili kuhusu usukuku na ukipatiaji lugha. Nadharia Teuzi ya Usukuku inaonesha kuwa vipengele vyote viwili, usukuku na ukipatiaji lugha hutokea kwa kuchochewa na hali fulani kama vile: motisha, ingizo la kutosha katika L2 na kuwepo kwa nafasi kubwa ya kuona na au kupata mrejesho wa athari za kimazingira katika zoezi la ujifunzaji na ukipatiaji L2 au lugha ya kigeni. Vitu hivi ndivyo vinawezesha ukipatiaji lugha (Chen, 2009). Hata hivyo, kwa mujibu wa Long (1997) hali ya ukipatiaji L2, au lugha ya kigeni, hushindikana baada ya balehe. Tafiti ambazo zimefanyika zinaonesha kuwa licha ya kuwa na vitu vyote hivyo; motisha, ingizo la kutosha na nafasi ya kuona matokeo kwa wajifunzaji wa L2 ambao tayari wamefikia balehe au zaidi hawawezi kufikia kiwango cha umilisi wa mzawa wa lugha ya kwanza (kuanzia sasa L1). Katika makala haya tunafasili dhana ya usukuku na kujadili aina za usukuku, kisha kutokana na aina hizo tunapendekeza mbinu za ufundishaji L2, au lugha ya kigeni, ili kuondokana au kupunguza hali ya usukuku miongoni mwa jamii ya Wakinga ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya pili.

¹ Nadharia Teuzi ya Usukuku ni fasili inayotokana na nadharia-tete ijulikanayo kama *Selective Fossilization Hypothesis*, kama ilivyobainishwa na Han (2009).

2.0 Fasili ya dhana

2.1 Usukuku

Dhana ya usukuku ilipendekezwa kwa mara ya kwanza katika taaluma ya isimu matumizi na Selinker (1972) kuwa ni tukio la kiisimu ambapo huwapata wajipatiaji L2 wenye umri zaidi ya ule wa balehe. Aidha, kwa mujibu wa Zheng (2010) usukuku ni miongoni mwa vizingiti au vikwazo katika mchakato wa ujipatiaji L2 au lugha ya kigeni. Kutokana na hali hiyo, ni jambo la welekea na au la muhimu kwa walimu na wanafunzi kuzingatia jambo hili. Pia, mbinu mwafaka na zinazofaa zaidi zinahitajika kutumiwa na walimu au wawezeshaji ili kuwasaidia wanafunzi kuondoka na hali hii.

Usukuku au ukomo wa ujifunzaji lugha kama ilivyobainishwa na Selinker (1972) ni tukio au jambo ambalo linawapata wajipatiaji L2 na au lugha ya kigeni. Usukuku unafasiliwa kuwa ni hali inayowapata wajipatiaji L2 ambao hushindwa kufikia kiwango cha umilisi wa mzawa wa lugha. Kwa maelezo rahisi kabisa usukuku ni hali ya kushindwa kumudu baadhi ya vipengele vya kiisimu vya L2 au ya kigeni, licha ya kuwa na ingizo la kutosha, motisha na kupata fursa ya kuona matokeo. Usukukishaji kiisimu ni tukio ambalo vipengele vya kiisimu, kanuni na mifumo ambayo wazungumzaji wa lugha fulani ya kwanza huendelea kuitumia katika lugha darajia/mpito pamoja na lugha lengwa bila kujali tofauti za kiumri, kiwango cha maelekezo au mwongozo utolewao na walimu. Ufafanuzi huu, unadokeza kitu muhimu kwamba licha ya maelekezo ya mwalimu kwa wajifunzaji wa lugha ya pili na ua lugha ya kigeni bila kujali umri wao, wajifunzaji au wapataji hawa huwa hawawezi kubadilika. Hata hivyo, Selinker (1996) amefasili dhana ya usukuku kuwa ni mchakato ambao mjifunzaji lugha hufikia ukomo katika lugha darajia au lugha mpito na hivyo kusitisha uendeleaji wa lugha darajia na kufanywa kuwa hali ya kudumu.

Tofauti na Selinker (1972, 1996) Ellis (1985) kwa upande mwingine anaona kuwa usukuku ni dosari au muundo/umbo sahihi la lugha darajia. Anaeleza kama kinukushi kifuatacho kama kilivyotafsiriwa katika Kiswahili kinavyoonesha hapa chini:

Usukuku utatokea wakati ambapo, mjifunzaji akiwa amefikia hatua ya maendeleo ambapo sifa X katika lugha darajia yake imechukua umbo kama lilivyo katika L2, kwa hiyo usukuku wa muundo au umbo sahihi utatokea. Na ikiwa mjifunzaji amefikia hatua ambapo sifa Y bado haifanani na muundo au umbo la L2 usukuku huchukuliwa kuwa ni dosari (Ellis 1985:48) (Tafsiri hii ni yangu).

Kulingana na dondoo hili, Ellis (keshatajwa) anaona usukuku una hatua mbili, kama mchakato ambapo kwake hiyo, sio usukuku bali jitihada za ujifunzaji lugha na matokeo ya mchakato huo. Matokeo ya miundo au maumbo yakifanana na L2 au

lugha ya kigeni hiyo ni dosari na ikiwa miundo au maumbo hayo yataendelea kutofautiana na L2 au lugha ya kigeni basi hizo ni dosari.

Hata hivyo, fasili ya Brown (1994) inatofautiana na zile zilizotolewa na Selinker na Ellis ambapo yeye anatazama usukuku kama ni matokeo ya athari hisivu chanya au hasi pamoja na mrejesho tambuzi (Brown, 1994:217). Yeye anahitimisha kwa kudai kuwa usukuku unaweza kuondolewa ikiwa, na ikiwa tu, wajifunzaji watapewa mrejesho wa athari hisivu chanya kama msingi wa kuwahimiza kufanya mawasiliano zaidi bila kupewa mrejesho wa tambuzi hasi. Hii ifanyike kwa kuhimiza urudiaji wa tena na tena. Msisitizo wa Brown (keshatajwa) ni kuwa usukuku unaweza kuondolewa kwa wajifunzaji bila kutilia mkazo athari hisivu za ndani. Aidha, Krashen (1982) anadai kuwa usukuku unaweza kuondolewa ikiwa tu mjifunzaji atapata ingizo la kutosha na kuwekwa katika mazingira halisi ya lugha anayojifunza atafikia kiwango cha juu cha umilisi wa lugha. Maelezo haya yanaonesha kuwa usukuku kama taaluma imeibua shule mbili za mawazo; moja usukuku unaweza kuondolewa na nyingine usukuku hauwezi kuondolewa.

3. 0 Aina za Usukuku

Kwa mujibu wa Selinker (1972) usukuku unaweza kuainishwa katika makundi makuu mawili ambayo ni Usukuku wa pekee (binafsi) na Usukuku jumuiivu (kundi). Uainishaji huu umezingatia kiwango cha athari ya L1 katika L2, yaani kiwango cha dosari ambazo zinakuliwa na usukuku. Aina hizi za usukuku zinafafanuliwa hapa chini kama ifuatavyo:

3. 1.1 Usukuku Pekee (binafsi)

Aina hii ya usukuku imeainishwa kwa kuzingatia vitu viwili; mosi, ruwaza ambamo dosari za aina fulani hutokea na ambamo dosari fulani zimechukuliwa au zimefikiliwa kama ni mfumo sahihi kulingana na kanuni na hujirudia. Pili, umilisi wa usukuku wa lugha, ambapo ni usukukuishaji wa lugha darajia katika uneni, muundo na msamiati. Aina hii ya usukuku kwa mujibu wa Krashen (1982) pia inajulikana kama usukuku wa muda (*temporary fossilization*). Hii inatokana na asili au chimbuko la usukuku huo.

3. 1. 2 Usukuku Jumuiivu (Kundi)

Hii ni aina ya usukuku ambao husababisha kuibuka kwa lahaja kutokana na usukukuishaji. Usukuku wa aina hii huwa umepata mashiko na kufikia kiwango cha kuunda au kutengeneza lahaja ya kwake ambayo ni tofauti kwa namna fulani na L1 au L2. Hii hutokea pale ambapo umilisi wa lugha sukuku huanza kukubalika na wanajamii wengi (*tend to be universal*) na kuwa tukio la kawaida na la kudumu katika jamii hiyo. Hivyo mfumo wa lugha ambao ni wa Kisukuku hutumiwa na jamii nzima. Aidha, aina hii ya usukuku kwa mujibu wa Krashen (1982) hujulikana

kama usukuku wa kudumu (*permanent fossilization*). Aina ya pili ya usukuku ndiyo inaelekea kuwa hujitokeza katika jamii ya Wakinga ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili ambayo ni sawa na hali inayotokea kwa Wachina wengi wanaojifunza lugha ya Kiingereza (Zheng, 2010).

Aidha, kwa kuzingatia asili ya usukukuishaji usukuku unaainishwa katika makundi mawili ambapo kuna usukuku wa kudumu na usukuku wa muda. Hata hivyo, kauli au uainishaji wenye kuzingatia asili ya usukuku unapingana kimtazamo na mawazo ya wanaisimu kama vile Jiang (2000), Lardiere (1998) na Long (1997) ambao wanadai kuwa kwa vyovyote vile iwayo bila kuzingatia motisha, kiwango cha ingizo, mwathiriano na mhamasisho kuna wakati ambapo ujipatiaji wa msamiati wa lugha ya pili au ya kigeni huwa unakoma au unasimama kuendelea kupata au kuimarika. Katika sehemu inayofuata tunagusia kwa ufupi dhana nzima ya lugha ya kigeni au lugha ya pili. Kisha tutahoji je, Kiswahili ni lugha ya pili au lugha ya Kigeni kwa jamii ya Wakinga?

4. 0 Lugha ya Pili

Stern (1983) anafasili dhana ya lugha ya pili kuwa ni ile lugha ambayo mtu hujifunza mbali na lugha mama yake na ambayo anaitumia kimawasiliano ndani ya nchi yake au mazingira ya mtu yule. Hivyo, kutokana na fasili hii jamii nyingi za Watanzania, Wakinga wakiwa miongoni mwao, lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili, kwani hujifunza na kuitumia lugha hii wakiwa tayari wana lugha zao za Kikabila na kuitumia ndani ya Tanzania au katika maeneo yao wanamoishi. Katika kushadidia wazo hili Mtesigwa (2009) anaeleza kuwa kutokana na ufafanuzi huu, tunaweza kusema kuwa Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi wa Afrika Mashariki ambao wana lugha za makabila yao na ambazo ndizo lugha mama walizozijua kabla ya kujua Kiswahili. Hata hivyo, utafiti kuhusu athari za lugha mama katika ujipatiaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili haujafanyika vya kutosha. Kuna haja ya kufanya utafiti mpana zaidi kuchunguza nafasi ya lugha mama katika mchakato wa ujipatiaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanajamii wa Kitanzania. Makala haya yanapendekeza mbinu za ufundishaji ili kuondokana na tatizo la usukuku kwa jamii ya Kikinga.

4. 1 Lugha ya Kigeni

Ni lugha ambayo mtu hujifunza na kuitumia lakini ni lugha ambayo wazungumzaji wake wako nje ya nchi au jamii anakokaa mwanafunzi yule (Mtesigwa, 2009:53). Anafafanua zaidi kuwa tofauti iliyopo kati ya lugha ya pili na lugha ngeni ni kuwa lugha ya pili huweza kuwa na hadhi ya kuwa lugha rasmi bila ya kulazimisha kwa kuwa ina uwezekano wa kuwa imesambaa kwingi katika jamii au nchi ambapo lugha ya kigeni haina hadhi hiyo isipokuwa pale ambapo nguvu za kiutawala au azma za kisiasa zimetumika ili kuipa hadhi hiyo. Tunakubaliana naye kwa kurejelea

hali halisi katika nchi ya Tanzania ambapo Kiingereza kinalazimishwa kinguvu kuwa lugha rasmi licha ya kuwa wanajamii wake hawaijui na haijasambaa sana. Katika sehemu inayofuata tunajadili aina za usukuku.

5. 0 Mbinu za Ufundishaji Lugha ya Pili ili Kuondokana na Usukuku

Katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili, ili kufanikisha michakato hii, kuna hatua au michakato ya namna tano ambayo haina budi kuzingatiwa katika utekelezaji wa ufundishaji wa lugha ya pili na au lugha ya kigeni ambapo ni: usasanyuzi kimahitaji (*need analysis*), ubunaji mtaala, utengenezaji vifaa, maelezo darasani na tathmini ya kozi (Zheng, 2010). Makala haya yanapendekeza njia mpya za ufundishaji lugha ya pili ili kuondokana na suala la usukuku kwa wanafunzi.

Mosi, kufanya Usasanyuzi wa mahitaji (*conduct needs analysis*); miongoni mwa wajifunza lugha kujua mahitaji ya wanafunzi haina budi kuchukuliwa kama hatua ya kwanza ya utafiti wa masomo na ujifunzaji. Huu unapaswa kuwa ndiyo msingi wa kwanza katika kubainisha mkakati wa ufundishaji lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari ambamo jamii ya Wakinga hukumbana na lugha ya Kiswahili kwa mara ya kwanza. Hii inaweza kusaidia hata kwa upande wa Walimu na wanafunzi. Kujua mahitaji ya lugha kwa wanafunzi kutawasaidia walimu au wawezeshaji kuteua zana zinazofaa, kubaini njia bora ya ufundishaji na kufanya maandalizi mengine mahususi. Wanafunzi wanakuwa na malengo mahususi ikiwa watajua mahitaji yao ya lugha wanayojifunza au wanayotaka kujifunza. Kwa kufanya hivyo watajifunza lugha kwa malengo ya namna fulani yenye kusukumwa na mahitaji yao. Kwa mwanafunzi mwenye kujua mahitaji yake atafanya bidii ya kujifunza lugha hiyo na kumwezesha kufikia umilisi wa mzawa lugha anayojifunza na hivyo suala la usukuku litakuwa limeondolewa.

Pili, kupima uwezo wa lugha lengwa alionao mjifunzaji. Upimaji wa uwezo wa lugha lengwa alionao mjifunzaji lugha hiyo unaweza kuhusisha matamshi, muundo, pragmatiki/muktadha, msamiati, sarufi na vipengele vingine kuhusu lugha hiyo. Nia ya kufanya upimaji huu, ni kujua kiwango alichonacho mjifunzaji na matatizo aliyonayo kuhusu lugha hiyo. Kwa kujua matatizo aliyonayo mwanafunzi, mwalimu ataweka mkazo katika kumsaidia mwanafunzi kuondokana na matatizo hayo. Upimaji unawasaidia walimu kuwaongoza wanafunzi katika maeneo ambayo ni tata na changamani sana kwao. Mwalimu akijua mahali palipo na tatizo kwa mwanafunzi atatafuta mbinu nyingi mbadala ambazo atazitumia ili kumsaidia mwanafunzi kuondokana na tatizo hilo. Hivyo, suala la usukuku kwa wajifunzaji lugha bila kujali umri, jinsi au mazingira litakuwa limeondolewa.

Tatu, kukuza mtazamo chanya kwa wajifunzaji lugha. Kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili na au lugha ya kigeni, tafiti za karibuni zimeonesha

kuwa mtazamo au hisia (*emotion*) ya wanafunzi kuhusu lugha kigeni au ya pili hayapaswi kupuuzwa. Zheng (2010:149) anafafanua kuwa hali ya mtazamo au hisia ya mjifunzaji kuhusu lugha anayojifunza vinaweza kuathiri moja kwa moja mwenendo na tabia ya mjifunzaji na matokeo ya mtazamo au hisia hizo kujidhihirisha wazi wazi. Mtazamo au hisia chanya kuhusu lugha mfano kuhusishwa na kupata kazi, heshima ndani ya jamii na au kuwa sehemu ya watu wa tabaka fulani kunatengeneza mazingira bora na motisha ya ujifunzaji lugha wakati mtazamo au hisia hasi mathalani lugha kuhusishwa na mabomu, umasikini, ugaidi na kutokuwa na nafasi yoyote kimataifa kunampotezea mwanafunzi umakini na motisha ya kujifunza lugha hiyo. Hivyo, suala la usukuku huwa ni sehemu ya mtazamo au hisia hasi. Kumotisha wanafunzi na walimu wao ni jambo ambalo halina budi kutiliwa mkazo katika ufundishaji wa lugha ya pili.

Nne, upandikazaji mbinu mahususi za ujifunzaji kwa wanafunzi. Kulingana na Chamot (1987), mbinu za ujifunzaji ni hatua, mikakati au njia za makusudi ambazo mjifunzaji huzichukua ili kufanikisha mchakato wa kujifunza na kuendeleza kumbukumbu zote kuhusu isimu na maelezo mengine ya kimuktadha. Kwa hiyo, mbinu za ujifunzaji ni muunganiko wa tabia, mtindo, mkabala na njia ambazo hupendelewa kutumiwa zaidi na wajifunzaji wa lugha ya pili. Mikakati ya ujifunzaji ni mfumo ndani wa kanuni na hatua za mfumo nje (*external procedure*) ambazo zaweza kuhusisha michakato miwili; ung'amuzi tambuzi na ung'amuzi bwete. Ung'amuzi bwete ndiyo kipengele muhimu sana katika kuondokana na suala zima la usukuku. Usahihi na uondokewaji na usukuku hufanywa katika hali ya ung'amuzi bwete. Muunganiko baina ya mfumo ndani wa kanuni za lugha na hatua zinazokusudiwa na mfumo nje kutawawezesha wajifunzaji lugha kujipatia kwa kiwango karibu sawa na wazawa wa lugha, hivyo kuondokana na suala zima la usukuku.

Aidha, mbinu au mikakati ya ujifunzaji inaweza kuainishwa katika kategoria tano kutegemea kiwango cha maarifa yapatikanayo na mchakato utokeo kwa kila hatua; ung'amuzi mpana utambuzi, athari za kijamii, mawasiliano na mkakati rasilimali. Zheng (2010:149) anashadidia hoja hii kama ifuatavyo:

Tafiti zimeonesha kuwa wanafunzi wa lugha wanaofanikiwa kuwa wamilisi wa lugha wanayojifunza ni wale ambao wanatumia vyema mbinu mkakati ya ujifunzaji (Tafsiri ni yangu).

Kwa hiyo, ni muhimu kwa kila mwanafunzi kuteua mbinu mkakati wake wa ujifunzaji ambayo inafaa kwake kwa ajili ya kuondokana na tatizo la usukuku. Tano, Uendelezaji wa umilisi wa lugha na mkakati wa kipragmatiki miongoni mwa wanafunzi Wanafunzi wanapaswa kujifunza maarifa mapana ya lugha lengwa bila

kusimama. Katika kutia ari ya mpango mkakati wa kimuktadha kwa wajifunzaji, maarifa ya kitamaduni ya lugha lengwa lazima yabainishwe kwa wanafunzi ili kuwawezesha wanafunzi kujua semo na namna mbalimbali za Kikinga na Kiswahili. Wakati huo huo uelekezaji wa mdomo katika lugha ya Kiswahili utumiwe na mwalimu ili kustahabali semo za lugha ya Kiswahili. Ni kwa kutumia mkakati na mbinu hizi ndipo wajifunzaji lugha wanaweza kukuza maarifa yao ya lugha na kuyatumia na hivyo kufanikisha mpango wa kuondokana na usukuku kwa kiasi kikubwa.

6.0 Mjadala na Tafakuri

Mjadala kuhusu suala la usukuku miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili na lugha ya kigeni mpaka sasa linaelekea kuibua shule mbili za mawazo. Shule moja ya mawazo inaamini kuwa ikiwa jitihada za makusudi na kuwapo kwa mahitaji ya msingi kwa wajifunzaji lugha ya pili au ya kigeni kunaweza kufanikisha kabisa kuondokana na tatizo la usukuku. Baadhi ya wataalamu wanaoangukia katika shule hii ya mawazo na mitazamo yao ni Krashen (1982) kuwapo kwa ingizo (*input*) la kutosha pamoja na uzamaji kindakindaki (*total immersion*) yaani hali ya mjifunzaji lugha ya pili au ya kigeni kuchangamana kwa kina kabisa na jamii ya lugha lengwa katika mazingira ya lugha lengwa ni mwarobaini wa usukuku. Aidha, Brown (1994) anabainisha; motisha ya mwalimu na jamii pamoja na maelekezo yanayofaa kwa wanafunzi ni tiba ya tatizo la usukuku miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili na lugha ya kigeni. Naye Chen (2009) anadai pamoja na mambo mengine mrejesho wa athari hisivu za wajifunzaji lugha toka kwa jamii ni utatuzi wa tatizo la usukuku. Hivyo, maoni ya jumla ya Krashen (1982) Brown (1994) Chen (2009) kuhusu usukuku ni kwamba usukuku unawezekana kabisa kukomeshwa bila kuzingatia suala la umri ikiwa motisha, ingizo la kutosha, uzamaji kindakindaki na mrejesho wa athari hisivu kwa wajifunzaji lugha utafanyika au utatolewa.

Tafakuri yetu kuhusiana na shule hii ya mawazo tukihusisha na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa jamii ya Wakinga ni kuwa pamoja na uzamaji kindakindaki (kutoka Makete) na kwenda kuishi katika miji kama Dar es Salaam, Tunduma na Mbeya ambako lugha ya mawasiliano ni Kiswahili ufahamu wetu unaonesha kuwa tatizo la usukuku kwa Wakinga lingali bado lipo. Mrejesho kadiri ya ufahamu wetu unatolewa vya kutosha na jamii inayowazunguka hasa kwa kuwaambia (kuwacheka/kuwatania) katika mazungumzo yao ya kawaida (soga) mfano sokoni, dukani, vijiwe vya biashara, vyombo vya usafiri, katika minada na hata wale waliopo shuleni juu ya namna jamii hii inavyozungumza kwa namna tofauti lugha ya Kiswahili lakini tatizo bado lipo. Aidha, licha ya motisha waliyonayo Wakinga ya kutaka kujua lugha ya Kiswahili ili waweze kufanya biashara, kwani jamii hii ni ya wafanyabiashara lakini bado tatizo lipo. Tunadhani kuna haja ya kuangalia

namna nyingine ya kuondokana na usukuku kama tulivyopendekeza hapo juu kuliko haya mambo matatu yanayobainishwa na wataalamu hawa.

Shule ya pili ya mawazo ni ile inayoona kuwa suala la usukuku ni tatizo la kudumu miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili na lugha ya kigeni. Baadhi ya wawakilishi wa shule hii ya mawazo ni Long (1997); Lardiere (1998) na Jiang (2000) kwa kutaja wachache ambao wanadai kuwa kwa vyovyote vile iwayo bila kuzingatia motisha, kiwango cha ingizo, uathiriano na muhamasisho kuna wakati ambapo ujipatiaji wa msamiati wa lugha ya pili au kigeni huwa unakoma au unasimama kuendelea kupata au kuimarika. Hoja hii inaimarishwa na tafiti ambazo zimekwisha kufanyika na kuonesha kuwa ujipatiaji na ujifunzaji lugha huwa haufanyiki kwa usahihi, haraka na ufasaha baada ya balehe, yaani mawazo yao haya yanajengwa kwa kuzingatia Nadharia tete ya Kipindi Maalumu (*Critical Period Hypothesis*) Ellis (1997) na Brown (2002).

Tafakuri yetu kuhusu shule au mtazamo huu wa mawazo ni kuwa ni uvivu wa kufikiri, kukatisha tamaa na kudumaza mawanda ya kufikiri kudhani kuwa ubongo wa mwanadamu hauwezi kupata maarifa ya lugha kwa ukamilifu baada ya balehe. Ikiwa lugha hufunzwa na mambo mengi pia hufunzwa. Kama mtu anaweza kujifunza mambo mengine kwa ukamilifu baada ya balehe kama vile umeme, uhandisi mitambo, mziki n.k ni wazi kuwa ikiwa zana za kujifunzia zitakuwepo za kutosha, muda, maelekezo, walimu waliobobea mjifunzaji lugha ataweza kujifunza lugha vizuri na kuwa mmilisi wa kiwango cha mzawa wa lugha hata baada ya balehe. Tafakuri yetu ni kuwa ujifunzaji lugha hufanyika karibu sawa na ujifunzaji wa vitu vingine hivyo inawezekana kupata maarifa ya lugha anayojifunza kwa kina sawa kama ilivyo kwa maarifa mengine. Mbinu tulizozipendekeza hapo juu taz. § 5.0. Aidha, ni udunishaji wa mawanda ya kufikiri na pengine ni kwenda kinyume kabisa na mawazo ya Gardner (1983, 1999a) ambayo tunafikiri bado yana mashiko kabisa ya *Multiple Intelligences*, ambapo watu duniani wana vipawa tofautitofauti kikiwemo hiki cha lugha. Je mtazamo huu unatoa hoja gani kwa watu ambao kwa mujibu wa Gardner (keshatajwa) kipawa chake ni lugha?

7.0 Hitimisho

Makala haya yalilenga kujadili mbinu mbadala ambazo zinaweza kutumika kufundishia lugha ya kigeni na lugha ya pili ili kuondokana na tatizo la usukuku kwa jamii ya Wakinga ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Njia au mbinu hizo zilizopendekezwa ni: mosi kufanya usasanyuzi wa mahitaji ya wajifunzaji wa lugha, pili kupima uwezo wa lugha lengwa walionao wajifunzaji, tatu kukuza mtazamo chanya kwa wajifunzaji juu ya lugha wanayojifunza, nne kupandikiza mbinu mahususi za ujifunzaji na tano kuendeleza umilisi wa lugha na mkakati wa kipragmatiki miongoni mwa wanafunzi. Aidha, katika kufanikisha

mjadala huu dhana ya usukuku imefafanuliwa, aina za usukuku pamoja na dhana ya lugha ya pili na kigeni imeelezwa ili kuleta uelewa mpana miongoni mwa wasomaji wetu. Kuhusu suala la usukuku tumeonesha kuwa kuna shule kuu mbili za mawazo; moja ikidai suala la usukuku ni tatizo la kudumu haliwezi kupatiwa majibu ya kuondokana nalo na shule nyingine ikidai kuwa usukuku unaweza kuepukwa ikiwa wajifunzaji watapata; ingizo la kutosha kutoka kwa walimu, jamii na mazingira. Pia, kama watakuwa na motisha ya kutosha, uzamaji kindakindaki katika mazingira ya lugha lengwa na mrejesho wa athari hisivu kutoka kwa jamii inayowazunguka wajifunzaji lugha. Tumeungana na shule ya mawazo ya pili nasi tumependekeza mbinu nyingine kwani kwa mujibu wa tafakuri yetu, mambo yanayoelezwa na wafuasi shule hii ni mazuri ili si hayo tu kwani yaliyobainishwa katika shule ya mawazo tapo la pili pekee hayatoshelezi kuondokana na tatizo la usukuku. Tumemalizia makala haya kwa kujadili kwa ufupi shule hizi za mawazo na kutoa tafakuri yetu, ambayo ni njia na mikakati bora ya ufundishaji lugha ya pili au lugha ya kigeni ni miongoni mwa nyenzo muhimu sana katika kuondokana na usukuku kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga.

Marejeo

- Brown, H. D. (1994). *Principles of Language Learning and Teaching* (Toleo la 3). Prentice Hall.
- Brown, H. D. na T. Rodgers (2002). *Doing Second Language Research*. Oxford, Oxford University Press.
- Chamot, A. (1987). 'The Learning strategies of ESL student.' In Wenden, A & J. Rubin (Wah). *Language Strategies in Language Learning*. Englewood Cliffs, N. J. Prentice Hall.
- Ellis, R. (1985). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford, Oxford University Press.
- Ellis, R. (1997). *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford, Oxford University Press.
- Gardner, H. (1983). *Frame of Mind. The Theories of Multiple Intelligences*. New York, Basic Books
- Gardner, H. (1999a). *Intelligence reframe. Multiple Intelligences for 21st Century*. New York, Basic Books.
- Han, Z. – H. (2009). 'Interlanguage and Fossilization: Towards an analytical model.' Katika V. Cook na L. Wei (Wah), *Contemporary applied linguistics* (Vol. I: Language teaching and learning pp. 137-162). London, Continuum.
- Jiang, N. (2000). 'Lexical Representation and development in a second language.' *Applied linguistics*, (27): 47-77.

- Krashen, D. S. (1982). *Principle and Practice in Second Language Acquisition*. Pergamon.
- Long, M. (1997 October). 'Fossilization: Rigor mortis in living linguistics systems?' Paper presented at SLRF '97 Conference, East Lansing, ML.
- Mtesigwa, C. K. P. (2009). "Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama lugha ya Kigeni: Haja ya kuzingatia Mkabaala wa Mawasiliano", katika *Kiswahili* (72), 52-67.
- Selinker, L. (1972). 'Interlanguage.' *International Review of Applied Linguistics*, (10): 209-230.
- Selinker, L. (1996). Fossilization: What we Think we Know, <http://www.nyu.edu/education/teachlearn/faculty/iselinker>.
- Zheng, Y. (2010). *On Some New Models of Instruction for Overcoming Fossilization in English Learning*. North China Institute of Science and Technology, China.